# *THIBITISHO NA USHAHIDI*

Asante, Ndugu Roy. Mungu akubariki...?...Asante. Asante, sana.

...amini tu.

2 Habari za jioni, marafiki. Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa katika Uwepo Wake.

3 Baba wa Mbinguni mwenye rehema, tunapokuja usiku wa leo, tena, kwenye tukio hili muhimu kuwazungumzia watu Wako, tunatambua haja kubwa ya wakati huu, nasi tunatambua u—u—uwezekano wa kumiminwa kukuu kwa Roho, tunaweza tu kukaribia kwa njia ifaayo, kwa hiyo tunakuja katika Jina la Yesu kuomba rehema.

4 Halafu basi, Baba, tunatambua usiku wa leo, tena, ya kwamba mbele zetu tunao walionunuliwa kwa Damu ya Yesu, na jinsi tunavyopaswa kushughulikia jambo hili. Na ni kazi kubwa mno kwa mwanadamu, kwa hiyo tunaomba, Bwana, ya kwamba utamruhusu Roho Mtakatifu aje sasa na kutuhudumia, na kutupa mambo tunayohitaji. Na kama shauku zetu ni mapenzi Yako, Bwana, tunaomba ya kwamba utatumwagia shauku zetu usiku wa leo, katika rehema Zake.

5 Waponye wagonjwa, waokoe waliopotea, wafariji wasiostarehe, na ujitambulishe Mwenyewe miongoni mwetu. Na naomba utufanyie jambo fulani, usiku wa leo, Bwana, jambo maalum.

6 Tunajua siku moja, huku wakija baada ya ule ufufuo mkuu wale wanawake waliokuwa wamerudi kutoka kaburini, nao walikuwa wakisema ya kwamba amefufuka, halafu basi Simoni akaja na kusema ya kwamba amefufuka, kisha watu wawili walikuwa wakienda zao Emau, ndipo Mgeni akatokea na kuzungumza nao safarini mwao, mwishoni mwa hiyo siku wakamkaribisha ndani. Mungu, huu ni mwisho mwingine wa siku, tunakualika uingie. Tunajua imekuwa ni Wewe ambaye umetusaidia siku nzima.

7 Ndipo mbele ya watu hawa wawili, Kleopa na rafiki yake, Ulifanya jambo fulani kama tu ulivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwako, kwa jambo hilo walijua ya kwamba umefufuka katika wafu na u hai miongoni mwa watu. Wakaharakisha kwenda kwa wenzao na kusema, “Kwa kweli, Bwana amefufuka.”

8 Basi, Baba, tunaomba ya kwamba utafanya jambo fulani usiku wa leo, katikati ya kukusanyika kwetu hapa, kama tu ulivyofanya kabla ya kule kusulubiwa, kuthibitisha ya kwamba

baada ya miaka elfu mbili ungali hai na unabaki Mungu yeye yule kama ulivyokuwa wakati huo.

9 Tunayakabidhi haya Kwako tunapoweka maombi yetu na imani yetu juu ya madhabahu Yako ya dhahabu, Bwana, na kuliitia Jina la Bwana Yesu, na kuomba ya kwamba utujalie haja zetu. Amina.

10 Mnaweza kuketi. Leo imekuwa siku isiyo ya kawaida sana. Asubuhi ya leo kwenye kiamshakinywa tulikuwa na wakati mzuri sana wa ushirika pamoja na ndugu na dada zetu. Na—nami nimehudhuria viamshakinywa vingi, lakini ndiyo mara ya kwanza niliyowahi kuwaona wakirudi na kusema, "Unataka kupakuliwa mara ya tatu? Kupakuliwa mara ya pili?" Siku zote ni ule mkahawa mdogo pembeni, nawe unakuta kwamba hujapata chakula cha kutosha, lakini nawaambia, tulikuwa na yubile ya ulaji bora sana asubuhi ya leo. Hakika tulikuwa nao, kweli tu—tulishiba.

11 Ndipo basi hao dada wakaendelea kukaribia, "Je, tukuongezee kahawa? Tukupe mayai mengine, ama...?" na, pande zote mezani. Bila shaka hakukuwako na sababu ya mtu yeyote kuondoka akiwa na njaa. Tulikuwa na wakati mzuri sana.

12 Halafu basi, nilifanya jambo ambalo sikuwahi kufanya hapo kabla, nilipata fursa ya kuzungumza katika sinagogi la Kiyahudi. Hiyo ilikuwa ndiyo mara ya kwanza niliyopata kuwa nayo. Wakati mzuri kweli. Na bila shaka tulikuwa na ushirika kule pamoja na—na...Ndugu Michaelson, nikijua yeye, ninaamini ana digrii ya udaktari nao wanamwita Dk. Michaelson. Nami nimemsikia kwenye *Majira ya Waebrania Wakristo*, mtu hodari kweli, aliye na mzigo kwa ajili ya watu wake bila shaka. Daima nimetamani kukutana na mtu huyu mzuri, lakini wakati huu alikuwa Palestina, naamini, pamoja na watu wake, na mzigo huo uko moyoni mwake. Wala sijawahi kupata majaliwa ya kukutana naye, lakini wanasema ana umri wa miaka sabini na sita. Nilipokuwa...

Mtu fulani aliniuliza hivi majuzi, akasema, "Ndugu Branham, una umri gani?"

Nikasema, "Loo, nimepita umri wa miaka ishirini na mitano."

Nao wakasema, "Umbali gani?"

Nikasema, "Imezidi miaka ishirini na mitano tu kwa ishirini na saba."

13 Kwa hiyo nilidhania nilikuwa ninazeeka, mpaka niliposikia jambo hilo, asubuhi ya leo, walio na sabini na sita na wangali wanaenda, ndipo nikajisikia kijana sana. Nikawazia, "Nina wakati mwingi zaidi bado, Bwana akikawia." Kwa hiyo wakati mwingine tunawaona hao askari wazee, na inafanya...

Mwenzake ameketi hapa nyuma yangu, sikuliona. Hao askari wa kale wanatufanya tujisikie wadogo basi, tunapowazia kwamba sisi, tumefanya jambo fulani.

14 Nilikuwa nikizungumza juu ya mzee wa thamani Ndugu Bosworth, wakati...Ni wangapi waliopata kumjua F. F. Bosworth? Loo, nadhani wengi wenu ninyi askari wazee mlimjua. Alipokuwa akifa, yeye...nilimwambia...nilishuka upesi kukutana naye, nami nikamwona akiinuka. Naye alikuwa na themanini na minne, naamini ndivyo. Alikuwa ndiyo kwanza atoke Afrika kwenye umisheni pamoja nami. Na maskini mikono yake mizee, maskini kichwa chake chenye upara, akainua mikono yake namna *hiyo*, akainyoosha, nami nikakimbia na kumkumbatia kwa mikono yangu. Nikalia, "Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli, wapanda farasi wake!"

Naye akasema, "Unajua, Ndugu Branham," akasema, "hii ndiyo saa adhimu sana ya maisha yangu."

Nikasema, "Je, unajua unakufa?"

15 Akasema, "Vema, siwezi kufa," kasema, "nimekuwa mfu kwa miaka sitini." Akasema...ndipo akasema, "Ninajiandaa tu kubadilisha makazi." Nanyi mwajua, ninyi nyote mliomjua, alikuwa mcheshi, naye alikuwa akizungumza nami pale, ndipo akasema, "La, Ndugu Branham," akasema, "katika huduma yangu yote, huu ndio wakati wangu wa furaha kuliko wote." Akasema, "Yote ambayo nimeishia, kwa miaka sitini iliyopita imekuwa ni Kristo, na dakika yoyote ataingia mlangoni, nami nitaambatana Naye." Loo, jamani!

16 Kabla hajafa, alikuwa kidogo katika hali ya kuzimia kwa saa chache, ndipo akasimama chumbani, amesimama pale huku amenyoosha mkono wake, akipeana mikono na waongofu wake wa miaka hamsini iliyopita waliokuwa wamevuka ng'ambo ya pili. Loo, jamani! "Maisha ya watu mashuhuri yote yanatukumbusha..." kama nilivyonukuu. Mimi...Mwisho wangu na uwe hivyo. Hiyo ni kweli. Mzee mtauwa, mtakatifu. Kwa hiyo huu ni wakati wetu, tutafufuka katika kizazi hiki, na itatubidi kusimama Hukumuni pamoja na watu hawa.

17 Hivi majuzi nilipotimiza mwaka wangu wa hamsini na tatu, nilimwambia mke wangu, nikasema, "Unajua, ningeninii... Vipi kama asubuhi, nitakapoamka, kama, niko kwenye siku yangu ya kuzaliwa, kama hapo angesimama Bwana Yesu, kama nilivyomwona Malaika wa Bwana amesimama pembeni, ile Nuru, chini ya Nuru hiyo angesimama Bwana Yesu, Naye angenijia, na kusema, 'Ungetaka nini?'" Ningesema, "Bwana, nipate kuishi muda mrefu zaidi kukutumikia Wewe." Naye angesema, "Umejaliwa, nitakurudisha nyuma sasa, mpaka uwe na umri wa miaka ishirini, ama kumi na minane. Uishi tena wakati uliosalia ukinitumikia Mimi."

18 Lakini hiyo haingekuwa sawa. Kama ningerudi kuwa na umri wa miaka ishirini, basi mke wangu. . .na hapa nina mwana mwenye umri wa miaka ishirini na saba, kwa hiyo hilo lisingekuwa sawa. Kwa hiyo basi nikawazia, "Vema, ninampenda mke wangu *sana*, na kumwona akiwa na umri wa miaka arobaini na mitatu na mimi kumi na minane, hilo lisingekuwa sawa."

19 Ndipo nikawaza, "Vema, ningeomba nini?" Nikawazia, "Vema, sasa, kama ningesema . . . Vema, ni—nisingeweza kuomba hilo kwa sababu, tena, hili hapa jambo lingine, mnaona, watu hawa niliowahubiria katika kizazi changu, itanibidi kufufuka pamoja na kizazi hicho. Mnaona? Itanibidi kusimama Hukumuni pamoja na kizazi hiki, kutangaza huduma ambayo nimehubiri, mnaona. Kwa hiyo nisingeweza kurudi katika kizazi kingine na kufa huku chini ya kizazi *hiki* nikiisha kukihubiria kizazi *hiki*."

20 Kwa hiyo nikawazia, "Vema, kadiri nijuavyo mimi ni mzima wa afya, kadiri nijuavyo lolote. Nami ningali na macho mazuri, ninasikia vizuri. Nami . . . Huduma aliyonipa, ninashukuru sana kwa ajili yake, ningeninii . . . Nimefanya vizuri nilivyoweza nayo. Kwa hiyo hakuna ila jambo moja ningeweza kufanya, na hilo ni kusema, 'Bwana Yesu, ninashukuru ya kwamba ni—niko jinsi nilivyo kwa neema ya Mungu.'" Hiyo ni kweli.

21 Inanikumbusha, si mahali pa kufanyia mzaha, siamini inapaswa kuwa *hapa* hata kidogo, bali halisemwi kwa mzaha, ila ni kutoa tu tamshi, kulikuwa na dada mweusi aliyekuwa katika moja ya hiyo mikutano mikubwa, naye akasema, "Vema," anasema, "Ninataka kutoa ushuhuda kwa utukufu wa Mungu." Akasema, "Si—siko jinsi ninavyopaswa kuwa," kisha kasema, "Siko jinsi ninavyotaka kuwa, lakini basi tena, ninajua siko jinsi nilivyokuwa." Kwa hiyo nilifikiri hilo lilikuwa ni zuri sana.

22 Nami ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo, kwamba siko jinsi nilivyokuwa. Nami nadhani sote tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo, ya kwamba hatuko jinsi tulivyokuwa, kwa kuwa tulipita kutoka mautini kuingia Uzimani. Na kama kuna watu hapa usiku wa leo ambao hawajui hilo, na wana hakikisho hilo, ninatumaini ya kwamba hutatoka nje ya milango mpaka nafsi hiyo imetiwa nanga katika mahali pa raha, isiabiri tena kwenye bahari zilizochafuka.

23 Sasa, jana jioni hatukuwaacha mtoke mpaka muda ulipokuwa umeenda sana, hapa muda umeenda sana usiku wa leo, lakini tutaenda nyumbani mapema. Sasa, sijajaribu ama kujaribu kuanza kuhubiri, kwa sababu, sihubiri kwa muda mrefu sana, wakati mwingine yapata saa sita wakati mimi . . . kitu kama hicho. Hivi majuzi nilihubiri kwa saa sita maskanini, kwa hiyo ninajua hamtaki nianze kuhubiri. Kwa hiyo nachukua tu Andiko dogo hapa, na kulisoma, na kutoa matamshi machache.

24 Na hata sijui kile . . . Je, Billy alisambaza kadi za maombi? Je, alisambaza kadi za maombi leo? Loo, kuna wengine waliosalia kutoka jana usiku. Vema, huenda tukafanyiza mstari wa maombi basi. Sijui atakalotaka tufanye. Na—napenda tu kukaa katika utamu wa Uwepo Wake, na halafu niingie chumbani, kisha nifanye tu yale anayoniambia nifanye. Mnaona? Hiyo ni kweli.

25 Nafikiri ya kwamba sote tunapenda hilo, nami nafikiri wahudumu wanapaswa kufanya hivyo. Sio kwenda kwenye karamu na kuchanganyikana na watu katika—katika mambo ya kijamii. Nafikiri tunapaswa kukaa katika utulivu, katika Uwepo wa Bwana. Na hilo limejaribu kuwa zoezi langu, kuingia kila alasiri saa tisa, kisha nisiongee tena mpaka nitakapoingia mimbarani usiku huo.

26 Sasa, usiku wa leo, kwa ajili ya somo la Maandiko, hebu na tusome katika Kitabu cha Mtakatifu, ama, cha Waebrania, hasa, samahani, mlango wa 6, kuanzia kifungu cha 13. Ninapenda kusoma Neno, kwa sababu ninajua Neno hili halitashindwa kamwe. Neno langu ni neno la mwanadamu, linaweza kushindwa, lakini kama nikisoma Neno hilo, basi ninajua ya kwamba hilo linatosha kuiimarisha mikutano, hata hapana . . . basi Maneno Yake hayatashindwa.

27 Sasa, hebu na tusikilize kwa makini sana, huku nikiwapa muda kidogo mpate kufungua Maandiko. Kumbukeni, ya kwamba haitupasi kamwe kuja kanisani kuigiza dini. Haitupasi kuja, kuninii tu, kujivalisha tendo la kidini tupate kwenda kanisani, hatuna budi kuja kuabudu katika Roho na katika kweli, hatuna budi kuwa waaminifu sana, lazima kweli tumaanishe kile kilichotuleta hapa. Siku zinazidi kuwa ovu, wakati ni mwovu, nasi tunataka—tunataka kutumia kila dakika, na hasa sana tunapokuwa katika nyumba ya Bwana.

28 Ninaangalia hapa, usiku wa leo, maskini mama aliyepindika, amenyanyuliwa, ameketi kwenye kiti cha magurudumu. Mtu mwingine anayeketi hapa, nilimwona mke wake, ama mtu fulani, kisha akapangusa tu uso wake, ameketi kitini. Huyu hapa mama ameketi hapa kwenye kiti cha magurudumu, miguu yake imenyanyuliwa, mama mkongwe ameketi nyuma kwenye kiti cha magurudumu.

29 Labda baadhi yao huko nje wenye ugonjwa wa moyo. Labda wamesikia mamia ya jumbe zikihubiriwa, bali wanajaribu kutafuta njia ya kupata afya usiku wa leo, wanajaribu kutafuta njia ya kuepukia. Na labda baadhi ya hao walio kwenye kiti cha magurudumu huenda wakaishi kwa miaka mingi bado. Huenda kuna mtu anayeketi hapo ndani mwenye kansa ambaye atakufa katika siku chache zijazo kama jambo fulani halitatukia. Ama labda mtu anayeketi pale mwenye ugonjwa wa moyo, wanaonekana kana kwamba wako sawa, lakini donge la damu

likizidi kusogea juu, huenda wakafa katika saa chache zijazo kama jambo fulani halitatendeka.

30 Na zaidi ya hayo yote, huenda kukawa na mtu anayeketi hapo asiyemjua Bwana Yesu. Nao wanajua. . .hawamjui katika nguvu za kufufuka Kwake, kusamehewa dhambi zao, wataangamia watakapokufa. Nao wanawajua wale walio na. . . huko nje labda wanaosimama katika hali ya kuhesabiwa haki, ambao hawajawahi kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, wanangojea hilo.

31 Kwa hiyo mnaona, kwa jumla. . .Nilisema, nilitoa tamshi, "Kama ningalikuwa na matone mawili ya Damu halisi ya Yesu katika bi—bilauri, jinsi ningeliishikilia moyoni mwangu na kulia! Nisimame pale nikiangalia kwamba sikujikwaa kuimwaga, ninapotembea nayo popote nilipokusudiwa kwenda nayo. Jinsi ningeangalia kila hatua, kwamba sikujikwaa, nikiiweka miguu yangu mahali inapopaswa kuwa!" Nikawazia, "Jinsi ningeshikilia hayo matone mawili ya Damu!"

32 Lakini mnajua, machoni pa Mungu, usiku wa leo, mbele yangu kuna kitu kikuu zaidi Kwake kuliko Damu Yake Mwenyewe, kwa sababu ni kile kilichonunuliwa kwa Damu Yake. Alimwaga Damu Yake kwa ajili yenu, nami hapa ninawashikilia katika kuisikiliza, usiku wa leo, Injili. Basi jinsi ninavyopaswa kuwaambia kwa makini ukweli halisi, kwa sababu Mungu atanifanya niwajibike kwa ajili yake kwenye Siku ya Hukumu, kuliko kama ningeichukua Damu, Damu halisi, na kuitupa ardhini. Ingekuwa adhabu kubwa zaidi kuwaelekeza vibaya watu, wale walionunuliwa kwa Damu Yake, kuliko ingelikuwa kuitupa hiyo Damu kutoka kwenye sinia niliyokuwa nayo.

33 Sasa, hebu na tuwe wanyofu sana, tunaposoma na kuchunguza na kuomba sasa. Katika mlango wa 6 kifungu cha 13 tunasoma:

> *Kwa maana Mungu alipompa Ibrahimu* ahadi*, kwa sababu yeye*. . .(Hebu nianze hilo tena, nilifungua kurasa mbili pamoja.). . .*kwa sababu yeye*. . .*alikuwa hana mkubwa kuliko yeye mwenyewe wa kumwapia, aliapa kwa nafsi yake,*
>
> *Akisema, Hakika kubariki nitakubariki, na kuongeza nitakuongeza.*
>
> . . .*hivyo kwa kuvumilia akaipata ile ahadi.*
>
> *Kwa maana wanadamu huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao, nacho kiapo hicho huthibitisha kile kilichosemwa na kukamilisha ubishi wote.*
>
> *Kwa njia hii Mungu, akitaka kuwaonyesha zaidi sana warithio zile* ahadi *jinsi mashauri yake yasivyoweza kubadilika, aliyathibitisha kwa kiapo:*

*Ili kwamba kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, tupate. . .faraja iliyo imara, sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yote yaliyowekwa mbele yetu:*

Bwana na abariki Neno Lake, tunapolizungumzia kwa yapata dakika kumi ama kumi na tano, tupate kuona kile, wakati anapotuongoza, cha kufanya.

34 Nilikuwa nikiwazia juu ya *Thibitisho Na Ushahidi*. Inaonekana kana kwamba mwanadamu daima anahitaji thibitisho, ama namna fulani ya ushahidi, na zaidi sana kwenye wakati huu, wakati wa wenye kushuku tunaoishi. Kila kitu hakina budi kuthibitishwa, lazima kiwe na u—ushahidi kwake. Na ninii—na ushahidi wa thibitisho hutupatia uhakika wa kile tunachotazamia.

35 Mtu anaponunua gari, hana budi kuwa na hati ya gari hilo, na ingawa hana gari kwenye gereji yake, kama ana hiyo hati, ni thibitisho kwake kwamba anamiliki gari hilo, kwa sababu anayo hati, ama, hatimiliki.

36 Halafu basi, kama tulinunua kipande cha ardhi, ingawa hatujawahi kuiona hiyo ardhi, hatujui chochote kuhusu hiyo ardhi, na hata hivyo tuna hatimiliki hakiki ya ardhi hiyo, ni mali yetu, kama tumeiona ama hatujaiona, ingali ni yetu. Hilo gari ni letu, kama tumeliona au la, hata hivyo tuna—tuna hatimiliki tuliyopewa, nasi tunayo wenyewe, kwa jina letu, kwamba hatimiliki hiyo inatuonyesha ya kwamba hilo gari ni letu; nayo hiyo hatimiliki hakiki inatwambia tunamiliki mali hiyo.

37 Sasa, katika Waebrania tunafundishwa tena, ya kwamba ile imani. . .Waebrania 11, "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Mnaona? Ni kuwa na hakika. Sasa, si tumaini; watu wengi huja wakiwa na matumaini. Lakini imani ni kuwa na hakika. Si kitu ambacho unatumainia. Wakati imani imeshikilia, una hakika, sio tu hadithi ya kubuniwa, umeshikilia kitu fulani, unajua jambo hilo, hakuna kinachokutikisa kutoka kwake, ni yako, una hakika, unayo mkononi mwako, unayo, ni mali yako.

38 Kwa mfano, kama nilikuwa nikifa kwa njaa. . .kwa. . . nilikuwa nakufa kwa njaa, na mkate ungeyakoa maisha yangu, nayo bei ya mkate ni senti ishirini na tano, kisha mtu fulani akanipa hizo senti ishirini na tano, sasa, naweza. . .Kadiri tu ninavyoweza kuona, na kujua ya kwamba ninashikilia hizo senti ishirini na tano, ambazo ndizo uwezo wa kununua mkate, ninaweza tu kufurahia hizo senti ishirini na tano kama vile ningeweza kufurahia nikiwa na mkate, mnaona, kwa kuwa tayari nina uwezo wa kuununua huo mkate.

39 Kwa hiyo hivyo ndivyo imani ilivyo. Imani ni kitu ulicho nacho, unajua unayo. Na unapopokea imani kwamba Mungu

*yuko*, basi, kwamba Mungu atakupa *hiki*, hata hivyo uponyaji wako huenda usiwepo, lakini hata hivyo, kitu fulani kimetia nanga ndani yako kinachokwambia ya kwamba itakuwa sawa, basi unaweza kuwa na furaha tu kadiri ulivyokuwa. . . unaweza kuwa na furaha vivyo hivyo huku umekalia kiti cha magurudumu, kana kwamba ulikuwa huko nje mtaani ukiruka-ruka, ukipaza sauti na kukimbia huku na huku, ukimsifu Mungu, kwa sababu tayari una ushahidi, tayari ni wako.

40 Mnaona, si hadithi ya uwongo, si mawazo, ni—ni kitu halisi. Na chochote ambacho, ni kitu halisi sio hadithi ya kubuni, ni kitu ambacho kwa kweli umekishika. Sasa, hapo ndipo watu wengi sana wanapokosa kuponywa, wana tumaini badala ya imani. *Unatumaini* kwamba utapona. Wewe—wewe, kwa namna fulani una imani ya kuwazia, kwa sababu unajisikia ya kwamba wewe ni. . .umeimiliki hiyo. Lakini wakati kweli umepata imani, ni hakika, ni kitu halisi. Ndipo unaishikilia hiyo, hicho ndicho kinachoileta.

41 Ambapo. . .Laiti ningalikuwa na imani hiyo ya mara moja, ambayo ningetaka kuwa nayo. Nasikitika sina hiyo. Njia pekee ninayotia nanga imani kuu ni wakati Yeye anaponiambia jambo fulani la kufanya, ama kunionyesha kulifanya.

42 Kama angetokea hapa jukwaani usiku wa leo, na angeniambia, “Nenda kwenye makaburi ya rais, kesho asubuhi saa nne ukamwite George Washington kutoka kwa wafu,” ningealika ulimwengu mzima uje uone ikitendeka. Naam, bwana. Kwa kuwa ninaamini yale niliyoambiwa, kwa sababu kamwe Yeye hajashindwa kuthibitisha lolote aliloniambia. Kwa hiyo ninaliamini, nikiamini, kwamba ni kweli, kwa sababu ni jambo lililojengeka.

43 Kote katika maisha, tangu nilipokuwa mvulana mdogo, maono yote, ya maelfu, hakuna hata moja lililokosea, kwa hiyo, ni kweli, hilo hunipa imani, nina imani katika yale Yeye asemayo.

44 Sasa, mara nyingi nimeshangaa kama wakati mwingine sikukiuka mipaka kwa kusema, “Mungu, nipe imani kuzungumza na *huyu*, nizungumze na *yule*, nizungumze na *yule*.” Sasa, tunatambua ya kwamba Bwana wetu Yesu, akiwa Imanueli, kamwe hakufanya hivyo, kwa kuwa Yeye alisema dhahiri katika Yohana Mtakatifu 5:19, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda,” (Sio, “analomsikia Baba akisema,” bali, “amwonalo Baba analitenda.”) “hilo atenda Mwana vile vile.” Unaona?

45 Hapana budi jambo fulani litukie linalokufanya uwe na u—ushahidi huu—huu, thibitisho hili. Sasa, kama Mungu alisema, “Itanyesha asubuhi,” isingekuwa vigumu kwangu kujiandaa kwa ajili ya mvua, kwa sababu ninajua itanyesha. Sasa, kama

tunaweza kubadilisha hilo kutoka kwa kuona ono, ama kusikia Sauti dhahiri ya Mungu. . . Lakini kubadilisha ikawa. . .

46 Njia ya kwanza ya kuwa na imani ni kwa kusikia Neno la Mungu lililoandikwa. Sasa, Mungu anapokuja miongoni mwetu na kujithibitisha Mwenyewe kwetu, katika kutupatia Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha na kufasiri, kutuma karama miongoni mwetu, namna hiyo, ama unabii unaosimama mahali *fulani*, na kusema jambo *fulani*, na kufanya jambo *fulani* na kulithibitisha wakati baada ya wakati, kwamba kamwe halishindwi, hilo linapaswa kutujenga kufikia mahali ambapo lingetufanya tulishikilie Neno hilo, ambalo tusingeliachilia. Inapaswa kuwa ni ushahidi papo hapo. Maadamu Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Mnaona?

47 Ninahofia kwamba mara nyingi kwamba—kwamba ha—hatusimami muda mrefu vya kutosha kuwazia juu ya hali tuliyomo. Sasa, karibu watu wote, ama, nasikitika nilisema hivyo, watu wengi katika ulimwengu wa nje, wanauangalia mkutano wa namna hii kama kitu fulani cha udanganyifu, bila kujua wanalosema. Nasi tutashukuru kwa hili, kwamba kumekuwako na uwakilishi mwingi wa uongo wa jambo hili.

48 Lakini kabla hujaweza kuwa na dola ya bandia, hapana budi kuwe na dola halisi ya kufanyiza hiyo ya bandia kutokana nayo, kama sivyo, basi hiyo ya bandia ndiyo ya asili. Unaona? Kwa hakika kadiri kulivyo na ya uongo, hapana budi pawe na ya kweli ambayo imetengenezwa kutokana nayo. Kwa hiyo kuna Roho Mtakatifu halisi, uponyaji halisi wa Kiungu, nguvu halisi za Mungu, imani halisi katika Neno, na hilo ndilo thibitisho, kitu ambacho kimetia nanga. Ni tukufu jinsi gani! Inathibitisha.

49 Mwanadamu hutafuta hilo, ni tabia ya mwanadamu, Mungu alimwumba mwanadamu hivyo, hivyo ndivyo Mungu alivyomwumba mwanadamu. Sasa, kwa hiyo basi, akimfanya mtu mwenye maumbile ya namna hiyo, Mungu hufanya jambo fulani kuridhisha shauku ya mtu huyo. Mungu ni Mungu mwema, kama vile Oral Roberts amesema mara nyingi. Yeye ni Mungu mwema, lakini usipeleke hilo mbali sana sasa, Yeye ni Mungu mwenye haki pia. Ndivyo hakika. Usimchukue Yeye mwema kupita kiasi, kama vile mtu fulani, mvulana tineja alivyosema si muda mrefu uliopita, "Mungu ni mwema sana Yeye hajali nifanyalo." Loo, naam Yeye anajali!

50 Kama kutokuamini Neno Lake, ku—kulielewa vibaya tu yodi moja ndogo, kulisababisha kila huzuni, kila ugonjwa, kila kifo, kila mtoto mchanga anayelia, anayekufa, kila makaburi, kwa sababu mtu mmoja alikosa kuamini sehemu tu ya Neno la Mungu, ilisababisha matatizo haya yote, msifikiri kwamba kamwe tutaacha sehemu yake moja ipite, tena, na kuingia pasipo kuamini chochote ambacho Mungu ameahidi.

51 Kwa hiyo, huenda nisiwe na imani, kama nilivyosema, kutembea kama Henoko alivyofanya, kutembea alasiri na kwenda Nyumbani pamoja na Mungu, lakini, laiti ningalikuwa na imani hiyo, bali kamwe sitasimama katika njia ya mtu mwingine, na kuwadhihaki hao walio na imani ya namna hiyo, nitawapenda, mtu ambaye ameshikilia imani hiyo.

52 Sasa, imani. Mungu alimwambia Ibrahimu hapa, akampa ahadi, kisha Mungu akamthibitishia ahadi hii, akampa ushahidi kwa kuapa mbele zake. Na jambo lisilobadilika ni kwamba Mungu hawezi kusema uongo, na isitoshe, wakati Yeye alipomwahidi, basi zaidi ya hayo, Yeye aliliapia.

53 Mungu akiapa kwa nafsi Yake. Inakubidi kuapa kwa mtu aliye mkuu kuliko wewe, wala hapakuwapo na mtu wa kumwapia aliye mkuu kuliko Yeye, kwa hiyo akaapa kwa nafsi Yake. Nayo ahadi ilikuwa kwa Ibrahimu na (*Na* ni kiunganishi.) kwa Uzao wake baada yake, si *wazao*, bali *Uzao* wake. Naye Kristo ni Uzao wa Ibrahimu, nasi, tukiwa ndani ya Kristo, Uzima wa Kristo ndani yetu unatufanya watoto wa Ibrahimu, nasi ni warithi pamoja naye sawasawa na ahadi.

54 Naye Ibrahimu, akiisha kuipokea hiyo ahadi, hakusita katika hiyo ahadi kwa kutokuamini, lakini alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu kwa muda wa miaka ishirini na mitano. Na karibu lilikuwa ni jambo lisilowezekana, wakati alipoipokea hiyo ahadi, maana alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye Sara, mkewe, alikuwa na sitini na mitano. Labda alikuwa amekoma hedhi kwa miaka mitano au kumi, naye alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye alikuwa akimsifu Mungu, sikuzote.

55 Natumaini hamfikiri ni kukufuru, bali ninaweza tu kuwazia sasa, Sara akiwa amepita wakati wa utu uke, naye angesema, "Sara," baada ya siku ishirini na nane za kwanza, "unajisikiaje, mpenzi?"

"Hakuna tofauti."

"Utukufu kwa Mungu, tutampata huyo mtoto kwa vyovyote vile." Mnaona?

Ndipo siku ishirini na nane zilizofuata, "Chochote kimetukia, Mpenzi?"

"Hakuna kitu."

56 "Utukufu kwa Mungu, itakuwa ni mwujiza mkuu zaidi sasa, bila shaka, kuliko ingalikuwa kama ingalitendeka mwezi uliopita." Mnaona? "Tutampata." Kwa sababu gani? Alimwamini Mungu, alikuwa ameshikilia kitu fulani. Angeweza kuliamini Neno la Mungu. Kushikilia, angeweza kuishikilia ahadi ya Mungu.

57 Sasa, tunaona basi mwaka ulipopita, hakuna kitu kilichotukia, miaka miwili, bado, "Utukufu kwa Mungu."

Sara akashona vijiatu vidogo, na maskini jicho ndege, mwajua, na kila kitu kikingojea. Alikuwa akingojea kwa sababu alijua ya kwamba mtoto huyu mchanga alikuwa yuaja, maana Mungu aliahidi hilo.

58 Na sasa tunapaswa kuwa Uzao wa Ibrahimu, tukinena kiroho, tukiwa ndani ya Kristo. Sasa, inatupasa kushikilia kila ahadi ya Mungu, na kuithamini kana kwamba imetimia tayari, kwa kuwa wakati Mungu amenena, kamwe hawezi kulighairi.

59 Sasa, Mungu anapofikia uamuzi, nao uamuzi ambao Mungu hufanya mara ya kwanza hauna budi kudumu vile vile daima, kwa sababu Yeye hana kikomo, Yeye ni mkamilifu, na maamuzi Yake ni makamilifu. Kwa hiyo, Yeye hawezi kusema, "Nilisema jambo hilo mwaka uliopita, lakini ninajua zaidi kulihusu mwaka huu." Mungu ni Mungu asiye na kikomo. Yeye ni mkamilifu, na kila uamuzi anaofanya ni mkamilifu, kamwe haimlazimu kuubadilisha, kwa sababu ni mkamilifu kwa kuanzia, kamwe haimbidi kuughairi.

60 Kwa hiyo, ninaweza kutoa ahadi, sijui, inanibidi kuighairi, bali Mungu hafanyi hivyo. Na kama Mungu aliitwa jukwaani kumponya mtu aliyekuwa mgonjwa, basi msingi ambao Mungu alimponyea mtu huyo, hana budi kudumisha jambo lile lile milele.

61 Wakati mtu alipopotea, njia Yake pekee. . .Yeye alifanya ma—maandalizi ya kumwokoa mtu huyo. Na juu ya msingi aliomwokolea, ungali unadumu leo hii, damu iliyomwagika. Kumponya mtu ilikuwa ni kwa imani, na hivyo ndivyo tu anavyoponya leo ni kwa imani kuliamini Neno Lake. Hiyo ni kweli kabisa.

62 Sasa, kwa hiyo Mungu baada ya kuthibitisha. . .Laiti tungalikuwa na wakati, lakini nilitoa ahadi. Baada ya Mungu kumpa Ibrahimu ile ahadi, ndipo akamthibitishia kwa kumpa tohara, ilikuwa ni ishara, na ilikuwa katika mwili wake.

63 Na sasa, ninazungumzia kusanyiko lililochanganyikana, lakini mimi. . .ninyi mnanichukulia kuwa ndugu yenu. Sasa, wakati Ibrahimu, akizeeka, nayo Biblia ilisema ya kwamba mwili wake ulikuwa kama uliokufa, angeweza kuangalia chini kwenye ishara hii katika mwili wake, naye alijua ya kwamba ilikuwa ni ishara ya Mungu ya kwamba Yeye angetimiza Neno Lake, tohara. Akaangalia ushahidi huo, akasema, "Mungu alitoa ahadi."

Sara akasema, "Lakini nina umri wa miaka tisini, nami nimeachana kwa mbali na tendo lolote la maisha."

64 Lakini basi Ibrahimu angeweza kugeuka na kuangalia ushahidi kwamba Mungu alisema, "Hii ni ishara." Naye Ibrahimu angeweza kumpa Mungu utukufu na kupata nguvu kuliko hapo awali, kwa sababu ilikuwa ni ishara, thibitisho kwamba Mungu atamjalia.

65 Sasa, Yeye pia aliahidi ya kwamba watoto wake wangekuwa wageni na kuwa katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne. Nao walikuwa katika nchi hii kwa miaka mia nne, watumwa, kama mbwa. Ilionekana, Mungu alikuwa amempa kisogo, bali ilikuwa ni kulingana na ahadi Yake. Hana budi kutimiza ahadi Yake.

66 Kama walitaka kumchukua mmoja wa hao wasichana wadogo wa Kiebrania na—na kumbaka, askari hao wa Misri, walifanya hivyo tu. Kama walitaka kumwua mmoja wa wana hao, walimwua tu. Wangemtupia maskini mkate wa kale uliojaa kuvu, nao wakaula la sivyo wafe. Nao, watumwa tu, nao wa—walilemewa na mizigo na kupigwa sana, na lilionekana ni jambo la kigeni kwamba Mungu angeruhusu jambo kama hilo. Lakini wakati mwingine Mungu hufanya mambo hayo, hutenda kwa njia za kipekee, bali daima Yeye hulitimiza Neno Lake.

67 Basi wakati wa ile ahadi ulipokaribia, nabii alishuka kutoka nyikani akiwa na BWANA ASEMA HIVI, Nguzo ya Moto ikimzunguka. Naye akashuka na kuwapa Neno la Bwana, kwamba alikuwa amesikia vilio vyao, na akakumbuka ahadi Yake, na kila mmoja wa hao waliotahiriwa.

68 Sasa, Yeye angekumbuka ahadi Yake, na kwa hiyo akawaambia ya kwamba kulikuwa na nchi ambamo wangeweza kulea watoto wao. Ilikuwa ni nchi ya kupendeza, ilikuwa nchi nzuri, iliyojaa maziwa na asali, wala hapakuwa na haja ya chochote kule, ilikuwa ni nchi ya thamani.

69 Kumbukeni, hakuna hata mmoja wao aliyewahi kuwa kule. Hawakujua chochote kuhusu nchi hiyo, bali iliwabidi kutenda kwa imani kwa ile ahadi, nao wakatenda kwa imani. Basi wakaondoka Misri chini ya uongozi wa Mungu, na nabii Wake aliyekuwa akiwaambia juu ya nchi bora zaidi.

70 Kwa hiyo wakatoka Misri, wakafika mahali paitwapo Kadesh-barnea. Ninaamini ilikuwa mahali pale ambapo Yoshua, shujaa mkuu miongoni mwao, aliende kule kuipeleleza nchi. Alivuka Yordani, kisha akaenda kwenye ile nchi nyingine, kisha akarudi na ushahidi kwamba nchi hiyo ilikuwa nzuri, kwamba Neno la Mungu lilikuwa kamilifu, ahadi Zake zilikuwa ni kweli. Naye alikuwa na ushahidi, thibitisho ya kwamba ile nchi ilikuwako. Alikuwa ameshikilia kitu fulani, kwamba hiyo nchi ilikuwa kama vile Mungu alivyoahidi itakuwa. Watu wawili walikuwa wamebeba kichala cha zabibu, watu wangeweza kukionja na kuona kwamba hiyo nchi ilikuwa nzuri. Ilikuwa ni thibitisho ya kwamba Mungu alikuwa ametimiza ahadi Yake.

71 Ndipo Israeli wakavuka Yordani na kuingia katika nchi ya ahadi, naye Yoshua akawagawia hiyo nchi. Walikuwa katika amani, walikuwa taifa, walikuwa na makanisa yao, walipanda mimea yao, wakawalea watoto wao, wakawapeleka kanisani,

nao waliishi kwa furaha. Ndipo Mungu akatia hofu katika mataifa hayo mengine yote, nao walikuwa watu mashuhuri.

72 Lakini hatimaye, baada ya miaka *kadha*, walianza kuchimba makaburi kule, kwa sababu wale mashujaa wa kale wa imani hatimaye iliwabidi washuke wafikie mwisho wa safari na wafe. Basi mawe ya makaburi yakaanza kutokea, na alama za vichwani, makaburi yakachimbwa katika nchi hii tukufu ambayo Mungu alikuwa amewaahidi. Iliwabidi kufa, bila kujali nchi nzuri waliyokuwemo, matunda mazuri waliyokuwa wakila. Lakini iliwabidi kufa.

73 Ndipo siku moja, akashuka Jemadari Mkuu, Bwana Yesu, Naye akaanza kuwaambia juu ya Nchi nyingine, "Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi, kama sivyo, ningaliwaambia. Nami nitaenda na kuwaandalia mahali, kisha nitakuja tena kuwapokea Kwangu; ili nilipo, nanyi mwepo." Maneno mengine, namna hii: "Umekuwa mwaminifu kwa huduma, bali huna budi kufa. Lakini kuna Nchi ambayo mtu anaishi wala hafi. Kuna Uzima baada ya mauti." Ni ahadi ya jinsi gani kwa watu! Lilikuwa la kushangaza sana, na liliwashtusha wengi.

74 Lakini Yeye alifika Kadeshi-barnea Yake. Kiti cha hukumu kilikuwa Kadesh-barnea, Naye akafika Kadeshi-barnea, Kalvari, ambapo Yeye alibeba ninii. . .Alizibeba dhambi za ulimwengu pale Kalvari.

75 Lakini pia alivuka Yordani, tunayoiita Yordani ya mauti. Alienda kwenye ile Nchi nyingine na alikuwa amekufa siku tatu mchana na usiku. Alikufa mpaka jua likaacha kuangaza, Alikufa mpaka dunia ikawa na fadhaa, ikaitikisa miamba kutoka milimani. Alikufa! Na katika siku ya tatu akafufuka tena, pamoja na ushahidi kwamba kuna Nchi ambamo mtu anaweza kuishi bila kufa. Alirudi kutoka Nchi hiyo. Kuna Uzima baada ya mauti.

76 Sasa, Yeye anawaambia wanafunzi Wake, "Nitawapa Arabuni ya hii, Nitawapa thibitisho la jambo hili," kama walivyofanya kwa Ibrahimu pamoja na tohara. "Lakini ngojeni huko juu Yerusalemu, mpaka mtakapopata lile thibitisho, mpaka mtakapokuwa na Ushahidi." Nao wakangojea, ndipo siku ya kumi kukaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, uliolijaza jengo lote walimokuwa wameketi, nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu. Ndimi za Moto zikawakalia, nao wote wakajazwa wakaanza kunena kwa lugha zingine kama Roho alivyowajalia kutamka.

77 Ilikuwa ni kitu gani? Ilikuwa ni Ushahidi kwamba Yoshua wetu, Yehova-Mwokozi, alikuwa amerudi kutoka kwa wafu na kutupa Ushahidi kwamba tunapokufa tunaishi tena Ng'ambo ya pili. Thibitisho, kuthibitisha, kutoa ushahidi wake.

78 Na sasa, leo, baada ya miaka elfu mbili, tungali tunaweza kuangalia nyuma, nasi tunaweza kuona mahali tulipokuwa wakati mmoja, chini katika uchafu wa dhambi. Nayo *dhambi* ni kutokuamini, hiyo ndiyo dhambi ya asili na ya pekee.

79 Mtu fulani alisema si muda mrefu uliopita, samahani, ilikuwa ni mwanamke, nilikuwa nikihubiri katika kanisa la Kimethodisti, nami nikasema, "Kunywa pombe si dhambi, kufanya uzinzi si dhambi, kusema uongo na kuiba si dhambi," basi lilimzidia sana maskini dada mmoja mkongwe wa thamani, naye akasimama na kusema, "Naomba uniambie, kwani dhambi ni nini?"

80 Nikasema, "Kutokuamini. Unafanya mambo hayo kwa sababu huamini, kama unaamini, mbona basi, usingeyafanya hayo. Ni sifa za kutokuamini." Nayo haki ni sifa ya imani, kwa sababu ulitia nanga katika imani hiyo, thibitisho, ushahidi.

81 Sasa angalieni nyuma mahali mlipokuwa wakati mmoja, sasa angalieni mahali ambapo mmeinuliwa kufikia sasa, kisha mkafa pamoja na Kristo, mkazikwa katika Jina Lake, mkafufuka pamoja Naye katika ufufuo. Kiroho, usiku wa leo, kulingana na Neno, sasa tumefufuka pamoja Naye, tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, huku kila pepo aliyeshindwa akiwa chini ya miguu Yake, tumeketi katika Uwepo ulio hai wa Bwana Yesu.

82 Loo, kama hilo halipaswi kukushikiza kitu fulani, kumwona Yeye akiwa na ushahidi uo huo, imani ile ile waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu, sasa ikifanya kazi, ikifanya mambo yale yale leo ambayo ilifanya daima! Kuona kuonekana kwa Bwana Yesu miongoni mwetu, na kuangalia nyuma, na kuona mahali tulipokuwa wakati mmoja, na sasa mahali tulipo sasa. Tulikuwa tumekufa wakati huo, na sasa tuko hai. Na kwa hakika kadiri tulivyokufa na kuzikwa pamoja Naye, tumefufuka pamoja Naye katika ufufuo, kwa kuwa tumefufuka kutoka *huko* chini. Amina. Sasa, ninajisikia kubarikiwa.

83 Kwa nini? Tumekufa, na maisha yetu yamefichwa katika Mungu kwa njia ya Kristo na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Ninaangalia nyuma na kuona mahali nilipokuwa wakati mmoja, *yule* William Branham alikufa miaka thelathini na miwili iliyopita. Na sasa sisi ni kiumbe kipya katika Kristo, tayari tumefufuliwa pamoja Naye na tumeketi pamoja Naye sasa katika mahali pa Mbinguni, pamoja na mamlaka ya Neno Lake lililoahidiwa, kwamba kila ibilisi atatutii, wala hakuna kitu kitakachothubutu. . .?. . . "Katika Jina Langu watatoa pepo, na kunena kwa lugha mpya, watashika nyoka, watakunywa vitu vya kufisha, wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

84 Hiyo ni ahadi Yake. Hili hapa thibitisho la ahadi Yake. Loo, hebu na tuungame udhaifu wetu! Na Mungu atupe nguvu na

imani katika Uwepo wenyewe wa Yesu Kristo ulio hai hapa usiku wa leo, Mwana wa Mungu.

85 Nilisimama pamoja na marafiki zangu wawili hapa, mnamo Februari, tulipokuwa huko Arizona, nasi tulikuwa huko nje mlimani, tulikuwa huko nje tukiwinda siku chache baada ya mkutano. Nasi tuliona nyota mbili, jinsi zilivyokaribiana, nami nikasema, "Labda kwamba zimeachana kwa umbali wa mamilioni ya miaka ya nuru, mbali kuliko vile tulivyo mbali nazo." Ndipo nikasema, "Kuwazia ya kwamba Mungu aliyeumba ulimwengu, Mungu Yule aliyeumba mfumo wa jua, Yeye aliyeziumba Mbingu na nchi, na kuziumba kwa Neno Lake lililonenwa!"

86 Kumbukeni, Neno ni wazo lililotamkwa. Mungu aliliwaza, ndipo alipokwisha kulitamka, halina budi kutukia, kwa kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu. Navyo vitu vilifanywa kwa vitu visivyoonekana. Ilikuwa ni Neno la Mungu, Yeye aliliwaza, ndipo akalinena, nalo halina budi kutimia. Ni mbegu inayokua, na, kiajabu hilo halina budi kuzaa majira yake.

87 Nasi tunaweza kuchukua Neno Lake, na kuona ya kwamba Yeye aliahidi, katika siku za mwisho ya kwamba angewavuta watu hawa na kufanya jambo lile lile alilofanya, kama alivyofanya katika siku za Sodoma, nasi tunaliangalia na kuona mambo haya, inatupasa kuishika ahadi ya Mungu, na kumjia Yeye, kwa kuwa tumetia nanga nafsi zetu katika mahali hapa pa raha.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

88 Bwana Yesu, thibitisho. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya Uwepo wa Yule wa Kiungu, usiku wa leo! Laiti watu wangalitambua mamlaka yao ndani Yake! Loo, jinsi lingekuwa ni jambo kuu, Bwana, laiti wangaliamini, wawe na imani! Jalia wao, usiku wa leo, waishikilie imani hiyo. Wamefundishwa jambo hilo, wamehubiriwa, imehubiriwa kwao, hasa, nao wameisoma kutoka katika Biblia, wameona wengine walioichukua.

89 Ee Mungu Mkuu Yehova, Mwenye Nguvu, uliyefanyika mwili na kukaa kwetu, sasa Wewe umefanyika mwili katika miili yetu na Roho Mtakatifu, hapa usiku wa leo, ukilihuisha Neno na kuhuisha ahadi ulizonena. Jalia, usiku wa leo, kwamba kila mwaminio apate kuliona na kuponywa, na kila asiyeamini apate kufumbuliwa macho yao kwa Uwepo wa Yesu Kristo, na thibitisho la kufufuka kwako.

90 Naye Mungu ambaye Yoshua, Yoshua wetu wa ile Nchi nyingine, Yule aliyetujia na kukutana na Kadeshi-barnea Yake kwa ajili yetu sisi sote...Nayo Kadeshi-barnea yetu ilikuwa kule madhabahuni usiku mmoja. Sasa tumehesabiwa kuwa tumekufa, nayo maisha yetu yamefichwa ndani Yake,

tukafufuka pamoja Naye katika ufufuo, tumeketi mkono Wake wa kuume leo katika mahali pa Mbinguni. Tujalie, Bwana, kwamba ufahamu wa watu upate kufunguliwa, nasi tutakupa Wewe sifa, katika Jina la Yesu.

91 Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa kwa muda kidogo tu, nitauliza swali hili, kwa uchaji. Wakati wetu unakwisha. Ninataka kuuliza swali zito, nami nataka ulijibu kutoka kwenye kilindi cha moyo wako. Ninakuagiza mbele za Mungu ya kwamba utafanya hivyo.

92 Kama bado hujaikubali ahadi hii ya Uzima wa Milele, nawe una hakikisho kamilifu na matendo ya Roho Mtakatifu maishani mwako, nawe ungetaka kuwa nao, naomba tu, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, kila mtu, inua tu mkono wako, useme, "Uniombee, Ndugu Branham, ninataka jambo hilo maishani mwangu." Mungu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mungu akubariki. Mungu akubariki, Mama. Ubarikiwe.

93 Vema. Mtu mwingine sasa, tunapongojea sema, "Ndugu Branham, uniombee, la—laiti ningalikuwa na thibitisho hilo moyoni mwangu, kwamba nimetiwa nanga katika Kristo, dhambi zangu zote ziko chini ya Damu, nami nina amani ipitayo ufahamu, nami ninajua ya kwamba mimi ni hai katika Kristo. Laiti ningeweza kusema hivyo, Ndugu Branham. Utaniombea?" Kuna wowote ambao hawajainua mikono yao, wangeinua mikono yao sasa? Mungu akubariki, wewe.

94 Bwana asifiwe. Hilo ni jema. Vema. Endeleeni tu kuinua mikono yenu, ninawaona huko nyuma kabisa. Ninangojea tu. Wahubiri, kila mtu, ombeni sasa. Mungu akubariki, anakuona, anauona uamuzi wako. Yeye anakuona, endelea tu kuomba. Anakuona, anakuangalia. Huko nyuma kabisa, ninauona, mwanangu, Mungu akubariki huko nyuma, huyu hapa. Endelea tu kuomba. Vema.

95 Baba yetu wa Mbinguni, umeona mikono yao ikiinuliwa. Kulingana na kanuni ya kisayansi, waliasi sayansi papo hapo, maana kulingana na sayansi mikono yao haina budi kuning'inia chini, nguvu za uvutano zinaishikilia pale. Lakini kulikuwa na roho ndani yao aliyefanya uamuzi, wakainua mikono yao, walikuwa tayari. Walijua ya kwamba kulikuwa na Kitu fulani kilichowazungumzia ambacho hakipatikani na mauti, Mungu wa Mbinguni, nao walijua hawakuwa sawa, na walitaka kuwa sawa, wakainua mikono yao, wakaamini jambo hilo. Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utawashughulikia sasa. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

96 Ni wangapi humu jengoni sasa hivi . . . ? Nilianza kutoa wito wa madhabahuni, lakini Roho Mtakatifu akanisimamisha. Hilo ni jambo la kigeni. Hakika ndivyo. Kuna jambo lingine, akasema, "Hujatoa Uwepo wa ninii Yangu . . . Thibitisho langu la Uwepo Wangu bado."

97 Ni watu wangapi hapa ndani, ambao hawana kadi ya maombi, huna kadi ya maombi, nawe unaamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliye hapa sasa, yuko pamoja nasi? Inueni mikono yenu. Ninyi nyote. Mnaona? Kila mahali tu. Asanteni. Hebu kidogo. Baadaye kidogo. . .

98 Omba tu na umwombe Mungu, "Bwana, ninaamini ya kwamba Maandiko yananiambia, mchungaji wangu amenisomea hilo, naye amehubiri juu yake, nimewasikia wengine, nao wananiambia ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Sasa, wanasema Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Bwana, naja, mimi ni mgonjwa, sikuwa hapa kuchukua kadi ya maombi, nami nitakugusa Wewe, Bwana. Na sasa, kama Ndugu Branham ametwambia ukweli, yeye hanijui, wala hajui chochote kunihusu mimi, ninakutaka unene kupitia midomo yake kama ulivyofanya kupitia midomo ya Kristo siku ile, na, kama Yeye alivyomwambia mwanamke kwamba, kuhusu kutokwa kwake na damu."

Basi wewe mguse tu Yeye. Na sasa, nilihisi ndani yangu. . . Ni karama, nami ninahisi. . . Ni kama tu kutia gia.

99 Na sasa, kama utamwamini na kumwomba, Mungu atakupa. Na kama atafanya hivyo kwa neema Yake usiku wa leo, tunaweza kwenda nyumbani na kusema, "Kweli Bwana amefufuka," kama wale waliotoka Emau, "nami nina thibitisho sasa, ya kwamba Yeye aliahidi ya kwamba 'Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.'" Kazi zile zile tulizonena habari zake jana usiku. Na Yeye ni yule yule jana, leo na hata milele, na Maandiko yamethibitishwa.

100 Nasi tunajua hakika ya kwamba tunaishi katika siku kama ya Sodoma na Gomora, kwa kuwa tunawaona wainjilisti ulimwenguni, nasi tunafundishwa ya kwamba Kanisa Teule ni Kanisa lililotolewa nje, na kutengwa na ulimwengu, ama mambo ya ulimwengu. "Nami niliona ishara ile ile aliyotoa pale, kabla ya kuteketezwa kwa Sodoma, na ni ahadi ya kwamba Yeye atauteketeza ulimwengu hivi karibuni sana."

101 Na basi kama Mungu atawafanya hivyo ninyi nyote mlio Sodoma kimbieni upesi mwezavyo, tokeni mje Kanisani. Vipi. . .? Kanisa gani? Watoto wachanga ambao ndiyo kwanza wazaliwe katika Kristo. Kuna Kanisa moja tu, hujiungi Nalo, unazaliwa ndani Yake. Mnaona? Mnaona? Ni kuzaliwa upya.

102 Mungu na ajibu maombi. Sasa hebu na tuchukue, safu tu, na hebu anene kwa safu. Kote kote kupitia hapo sasa, ambao hawana kadi ya maombi, sasa, kama una kadi ya maombi, usiinue mkono wako, wale wasio na kadi ya maombi, mahali popote katika safu hii ya mkono wa kulia, inua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, ninaomba." Kama hujiombei

mwenyewe, mwombee mtu mwingine, chochote utakacho, kuwa tu na haja, omba. Vema. Mungu awabariki.

103 Sasa, angalia huku na useme moyoni mwako, "Bwana Yesu, ninaamini Neno Lako." Nayo Biblia inasema, katika Waebrania mlango wa 4. . . Sasa, tunajua, kabla hatujasema jambo hili, ya kwamba Yesu alikuwa ni Neno la Mungu lililofanyika mwili. Hiyo ni kweli? Biblia inasema, katika Waebrania 4, ya kwamba "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, likigawanya mafuta ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo."

104 Hiyo ndiyo sababu angeweza kuwaangalia na kusema, "Imani yako imekuokoa." Akalishika. Hilo ni Neno. "Nanyi mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu. . . " Usichanganye fundisho fulani la kimadhehebu, la kujibunia ndani yako, dumu safi, usiyeghoshiwa pamoja na Neno. "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo. Kwa kuwa Neno ni Mtambuzi wa mawazo ya moyo." Amini tu sasa, amini. Angalia kama Yeye anathibitisha yale nimesema kwamba ni kweli.

105 Iweni tu na kicho kwa dakika moja. Nikihubiri, na halafu, ni—nilitaka kutoa wito wa madhabahuni, bali Yeye Ndiye aliyeniita kufanya jambo hili, kwa hiyo hakika Yeye atanisaidia.

106 Naam, hiyo hapo. Huyo mama aliyeketi papo hapo nyuma, amevaa nguo nyekundu ya chungwa hivi, akimwombea mama yake, anatikisa kichwa chake *hivi*. Ana nywele nyeusi. Simama tu kwa dakika moja, Mama. Naam. Je, una kadi ya maombi? Huna. Jambo la kigeni kabisa lilikupata muda mfupi tu uliopita, ulijisikia halisi, kama kitu Fulani kinyenyekevu sana na kitamu karibu nawe. Ninaangalia moja kwa moja kwenye Nguzo hiyo ya Moto, moja kwa moja juu ya mahali ambapo mwanamke huyo amesimama.

107 Anamwombea mama yake. Mama yake hayupo hapa. Unaamini Mungu anaweza kuniambia mama yako ana shida gani? Ungeamini basi, kwa moyo wako wote? Ana ugonjwa wa moyo. Hiyo ni. . . Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, utakapoenda, mkute akiwa mzima. Amina. Mungu akubariki.

108 Unaamini? Katika safu hii ombeni, na kusema, "Bwana Mungu, maskini mhubiri huyo aliyesimama hapo hanijui, bali Wewe unanijua, nami ninagusa vazi Lako. Nijalie, Bwana, nijalie."

109 Hapa, moja kwa moja juu ya mtu mweusi aliyeketi hapa mwishoni mwa safu, anakabiliwa na upasuaji. Wewe, Bwana. Je, una kadi ya maombi? Huna. Huhitaji moja. Ugonjwa wa kibofu. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya ugonjwa huo wa kibofu? Unaniamini mimi. . .? Huyo hapo roho mwema papo hapo. Je, unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, ama, mtumishi Wake? Samahani, hilo huwakwaza watu. Unaamini?

Kwa moyo wako wote? Asante, Bwana. Hiyo ndiyo njia ya kuwaamini hao ambao Mungu aliwatuma. Ukitaka kufanikiwa, unajua kile Yeye alichosema ufanye. Bw. Benton, hilo ndilo jina lako, wewe hutoki hapa, unatoka kwenye mji unaoitwa Compton. Kama utaamini kwa moyo wako wote, imekwisha. Mungu akubariki.

Mnaamini?

110 Moja kwa moja nyuma ya mstari kuna mama mmoja. Anamwombea mpendwa, naye mpendwa huyo ana kiharusi, ni mzee. Huyo mama, Bibi Dawson, amini. Je, una kadi ya maombi, Mama? Huna. Sikujui, hatufahamiani, bali unamwombea mpendwa, na huyo mpendwa ana kiharusi, ni babu. Naye haishi hapa, anaishi mahali panapoitwa Bakersfield, naye ni mhudumu wa Injili. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

Unaamini? Kuwa na imani sasa.

111 Mama huyu aliyeketi hapa, akiomba, ana ugonjwa wa moyo, aliyeketi papo hapo nyuma, akiniangalia. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, Mama? Huyo mama mwenye mvi, akitikisa kichwa chake, moja kwa moja hapa. Vema, wewe, naam. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Je, una kadi ya maombi? Huna. Huihitaji. Ugonjwa wako wa moyo umekuacha sasa. Sasa, angalia, wewe endelea. Sasa, kama ukipoteza imani . . . Unajisikia vizuri, sasa hivi. Imani inayoweza kukufanya ujisikie sawa, sasa hivi, inaweza kukudumisha hivyo mradi tu unaidumisha imani hiyo. Usitie shaka. Amina.

112 Ninaona, iko papa hapa, juu ya mama huyu katika ninii hii. . .nyuma tu ya yule mama kwenye kiti cha magurudumu. Ni mwanamke huko nyuma. Naam, ni ma—mama fulani, mama huyu aliyeketi pale akimwombea mama ya—yake, aliyeketi karibu naye hapo. Unamwombea. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yake? Hivi wewe . . .? Je, una kadi ya maombi? Huna. Vema. Kama unaamini kwamba ugonjwa wa Bright utamwacha, utamwacha. Weka mkono wako juu yake, na uamini kwa moyo wako wote, naye atapona. Usitie shaka.

113 Loo, Yeye ni Ua la Uwandani, Ninyoro ya Bondeni! Thibitisho ya kwamba Yeye yu hai milele! Unaamini hilo? Je, ungetaka kuja wakati huu, kama mwaliko? Wote, kila mtu aliyekandamizwa na dhambi, utakuja sasa na kusimama hapa? Kama atanijulisha shida za watu, na yote kuhusu mambo haya, Yeye ananiambia sasa, kuna watu hapa ndani wanaopaswa kuja na kuyasalimisha maisha yao Kwake, mtakuja?

114 Inuka moja kwa moja kutoka kwenye kiti chako, wewe uliyeinua mkono wako. Njoo papa hapa na usimame. Wewe ambaye hujazaliwa mara ya pili, hujui lolote kumhusu Mungu na mambo haya, mtakuja sasa? Katika Uwepo Wake, kama mnaamini ya kwamba huyu ni Roho Mtakatifu, njoni sasa

tunaposimama na kuimba wimbo fulani. (Chochote wewe, ulichochagua, chochote.)

115 Na tunaposimama na kuimba wimbo huu, ninawatakeni mje sasa hivi, kabla hatujaendelea na ibada ya maombi. Hebu—hebu tuone. . .tumalize hili, maana Kitu fulani kilisema, wakati uo huo tu, "Fanya wito wako wa madhababuni sasa. Ulihubiri juu ya thibitisho, nawe huyu hapa, nimethibitisha ya kwamba nipo hapa." Amina.

116 Kama hamwezi kuona hilo, enyi marafiki, ninyi ni—ni vipofu, kuna kasoro fulani, hamna tumaini, wakati Mungu, akifanya jambo kama hilo. Ni wangapi wanaoamini Yeye yupo hapa? Ni wangapi wanaoamini kwamba ni Yeye? Nina hakika, kwa moyo wangu wote, kwa Biblia yangu, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, yule MIMI NIKO Mkuu, sio, "Nilikuwa," MIMI NIKO, yuko hapa akitenda katika mwili wa watu Wake, jambo lile lile alilofanya alipokuwa katika mwili wa mwanadamu hapa duniani. Haleluya! Ninaamini kwa moyo wangu wote. Mnaamini jambo lile lile?

117 Wakati sote tumesimama, njoni huku kila mtu, ningetaka kukupa mkono, nisimame hapa na kuwagusa, na kama unataka kumpata Kristo, omba msamaha wa dhambi yako.

> . . .natoa yote,
> Natoa yote,
> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.

Hiyo ni kweli. Shukeni moja kwa moja mje huku.

> Natoa yote,
> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.

118 (Hebu kidogo.) Kemeo la Roho Mtakatifu: Wakati mikono mia mbili au zaidi ilipoinuliwa dakika chache zilizopita, na wakati nilipotoa wito wa madhababuni, yapata watu mia tatu walitoka mlangoni, wakipitia upande ule mwingine, ndipo mvulana mdogo, wawili wao, wamekuja na kupiga magoti hapa kando. Nena kuhusu Sodoma na Gomora, nena kuhusu Siku ya Hukumu ambayo imekaribia, wakati Mungu katika rehema Zake, akionyesha kila kitu anachoweza kufanya, huku watu wakiwa wagumu sana wa Injili mpaka wanaondoka moja kwa moja mbele ya Roho Mtakatifu!

119 Unasema, "Hao hawakuwa watu. . ." Naam, ni watu waliopaswa kuja. Kama ninajua *Hii* ni nini, ninajua *hao* walikuwa ni akina nani. Naam, bwana. Roho Mtakatifu alihuzunika vibaya sana. Na huenda ulifanya hivyo kwa mara yako ya mwisho, ninatumaini sivyo, lakini huenda ulifanya hivyo kwa mara yako ya mwisho. Hii ni ya Bwana. Basi kumbukeni tu, mimi si tapeli, mimi si mlokole, ninajua mahali nilipo hasa, na yale ninayozungumzia. Naam.

120 Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho, si ajabu Los Angeles na ulimwengu wote uko njiani kuelekea kuzimu, si ajabu mnaivishwa kwa ajili ya bomu la atomiki. Enyi watoto wadogo, jitulizeni kando ya msalaba na mkae hapo, saa imewadia.

121 Nilienda Bombay, India, hapa si muda mrefu uliopita, na kuchukua gazeti, kasema, "Ishara ya tetemeko la ardhi imekwisha." Siku mbili au tatu kabla ya kutokea kwa tetemeko la ardhi, maskini ndege wote waliruka kutoka kwenye viota vyao vilivyokuwa kwenye kuta za miamba, kondoo wote na ng'ombe waliosimama kando ya kuta, wote walienda kondeni, wakasimama karibu wakiegemeana, kwa namna fulani wameegemeana *hivi*, mmoja kwa mwingine, wakifanyiana kivuli.

122 Kwa nini? Kulikuwa na silika, Kitu fulani kiliwaambia ya kwamba tetemeko la ardhi linakuja. Tetemeko la ardhi lilizitikisa kuta hizo zikaanguka. Kama wangalikaa mle ndani, wangeangamia. Lakini sasa, baada ya tetemeko la ardhi kwisha, walirudi kwenye kuta tena, zilizokuwa zimesimama.

123 Sasa, hebu nikwambie, rafiki, kwamba Mungu wa Musa, Yule aliyeweza kuwaingiza katika ile safina, angeweza kuwaondoa kwenye hizo kuta. Na kama Mungu, kwa silika katika ndege, angeweza kumwita kutoka hatarini, ni zaidi sana jinsi gani anapaswa kuwaita wanadamu, ambao wamevuviwa na Roho Mtakatifu? Ni jambo ovu jinsi gani! Ni kizazi cha zinaa jinsi gani! Ni mahali paovu jinsi gani tunapoishi! Ni taifa lenye dhambi na lisilomcha Mungu jinsi gani tulilo nalo, walioachwa na Mungu, wanaomchukia Mungu, wanaotafuta ishara, wanaofuata upepo, waigaji, wanaojilinganisha kimwili, wakiongozwa na upuuzi mtupu, na wanaokaribia mwisho wa safari! Ninasema hayo katika Jina la Bwana.

124 Mara nyingine tena nitaita, ni juu yako kujibu. Vema.

> Natoa. . .(Njoo, ewe mwenye dhambi, katika
> Uwepo wa Mungu.)
> . . .natoa yote,
> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.
>
> . . .natoa, (natoa yote.)
> Natoa, (. . .?. . .natoa yote.)
> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.

125 Kumbukeni, siku moja nitasimama mbele zenu mbele za Mungu, kizazi hiki kitakapotokea. Ninawapa, usiku wa leo, uhuru kutoka kwa dhambi zenu, kupitia Yesu Kristo, nawapa amani ipitayo ufahamu, ninawapa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kama mtafuata maagizo ya Biblia ya Mungu. Mbona usije, uupokee?

> Na. . .

Wakati wahudumu wakishuka, wakiweza, wakiwazunguka watu hawa.

> Natoa yote,
> Natoa yote,
> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.
>
> Natoa, (natoa yote.)
> Natoa, (natoa yote.)
> Loo, yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa . . .

Hebu na tuinue mikono yetu sasa na kumsifu Mungu, kila mmoja wetu. Yasalimishe maisha yako.

126 Bwana Yesu, pokea matoleo yetu, Bwana, na ninii . . . watu hawa walio madhabahuni, wapokee, katika Jina la Yesu Kristo.

62-0621E Thibitisho Na Ushahidi
Great Western Exhibit Center
South Gate, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org